# Kanuni za Kina za Uhifadhi na Ufuatiliaji wa Mazao ya Bahari kwa njia ya Kielektroniki (eCDT)

**Toleo la 2.0 Septemba 2023**



Photo Credit Alinamd adobestock.com

SALT
SEAFOOD ALLIANCE FOR LEGALITY & TRACEABILITY

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE · WALTON FAMILY FOUNDATION · the David & Lucile Packard FOUNDATION · GORDON AND BETTY MOORE FOUNDATION · FISHWISE

## Kuhusu SALT

Umoja wa Ufuatiliaji na Uhalalisho wa mazao ya bahari (SALT) ni muungano wa serikali mbalimbali ulimwenguni, ikiwemo viwanda vya uchakataji mazao ya uvuvi pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali. Umoja huo umekua ukishirikiana katika kutafuta ufumbuzi wa matumizi endelevu wa mazao ya bahari, hasa kwa kujikita katika ufuatiliaji wa mnyororo wa usambazaji wa vyakula. SALT in taasisi binafsi yenye ubia na USAID pamoja na Packard, Moore, na Walton Family Foundations (Mfuko wa hisani wa familia), miradi yake inatekelezwa na FishWise (Taasisi inayojihusisha na utoaji ushauri kuhusiana na uzalishaji endelevu wa mazao ya bahari), kama mshauri mwelekezi wa mazao endelevu ya bahari. FishWise itaendelea kutoa huduma muhimu za kuitisha jumuiya ya SALT mwaka wa 2024. Hii ni pamoja na kuunda mikakati ya ufuatiliaji na kusaidia serikali, biashara na mashirika yasiyo ya kiserikali duniani kote kuweza kutumia Kanuni za Kina za Ufuatiliaji.

## Kuhusu FishWise

FishWise ni miongoni mwa wataalamu nguli ulimwenguni waliobobea kimataifa katika ufuatiliaji wa mazao ya bahari na kupunguza hatari dhidi bidhaa haramu za bahari na zisizo na maadili. Kama shirika, linachunguza, linajaribu, linatekeleza, na kusambaza mazoea ya biashara yenye uwajibikaji ili kuboresha uwazi na usimamizi wa uwajibikaji wa minyororo ya usambazaji ya bidhaa za bahari ulimwengu ni na kupunguza athari hasi kwa mazingira na ukiukwaji wa haki za binadamu. Kwa kutumia mazoea bora na zana za hivi karibuni, FishWise inafanya kazi ya kudumisha mifumo ikolojia ya bahari na watu wanaotegemea mifumo hiyo kwa kubadilisha minyororo ya usambazaji wa mazao ya bahari duniani kote. FishWise inamaono kuhusu tasnia ya mazao ya bahari, kushirikiana na serikali na jamii, inachukua jukumu kamili kwa watu na rasilimali bahari ambazo inategemea, ili kwamba:

- **BAHARI** (ikiwa ni pamoja na mifumo ya mazingira ya baharini na maji safi ambayo ni muhimu kwa kusaidia maisha kwenye sayari hii) zinarejeshwa ili ziwe na uzalishaji zaidi na utofauti wa viumbe hai wakati zinatoa chanzo muhimu cha protini bora kukidhi mahitaji ya idadi ya watu inayokua duniani.
- **WATU** (ikiwa ni pamoja na mamilioni ya wanawake na wanaume wanaovuna, kuzalisha, kusindika na kuuza mazao ya bahari) hunufaika na kusitawi katika tasnia yenye usawa na haki na mazingira mazuri ya kazi kwa wote.
- **BIASHARA ZA MAZAO YA BAHARI** (zilizoundwa na wazalishaji wa kiwango kidogo na kikubwa, wasindikaji, wasambazaji, na wanunuzi wanaotoa chakula na kipato) ziendelee kuwa na uwezo wa kifedha kwa vizazi vijavyo.

Ripoti hii imewezeshwa kwa msaada wa Watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo la Kimataifa(USAID). Yaliyomo katika ripoti hii ni jukumu la FishWise na hayawakilishi maoni ya USAID au serikali ya Marekani.

# Yaliyomo

Misingi na Mwongozo wa Njia 2.0-2023 Simulizi ya Mabadiliko. . . . 1

Utangulizi . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 3

Kanuni za Ufuatiliaji . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5

Muhtasari . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

Kanuni za Kina za Uhifadhi na Ufuatiliaji wa Mazao ya Bahari kwa njia ya Kielektroniki (eCDT) . . . . . . . . . . 7

Kuzifikia Kanuni . . . . . . . . . . . . . . . . . 8

*Kuanzisha* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9

*Kuunda* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 14

*Kutekeleza* . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 22

Tumia Kanuni . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 26

# Misingi na Mwongozo wa Njia 2.0-2023 Simulizi ya Mabadiliko

Kwa jitihada za kuendeleza Misingi na Hatua za Njia kuwa na umuhimu na manufaa kwa waundaji wa programu za ufuatiliaji, watendaji, na watumiaji, tumefanya marekebisho kwenye yaliyomo na rasilimali zinazopatikana kwenye tovuti hii. Misingi na Hatua za Njia zote ni "hai," maana kwamba zitaendelea kuboreshwa, kubadilishwa, na kufanyiwa marekebisho yanapohitajika. Tutaendelea kutambua na kujumuisha rasilimali husika kwa Njia ili kusaidia utekelezaji kadiri inavyowezekana.

**Toleo la 2.0 Masasisho yanajitokeza:**

- Mapungufu/Mapengo yaliyobainika wakati wa uzinduzi wa Kanuni.
- Maoni kutoka kwa wadau wa uvuvi na jamii inayo zalisha mazao ya bahari ambao wana uzoefu wa kutumia Kanuni kwenye kazi zao (tazama "Mifano ya Kesi" kwa taarifa zaidi kuhusu miradi hii).
- Tathmini ya ndani.
- Mabadiliko ya jumla katika miongozo na kanuni za ufuatiliaji wa mazao ya bahari.

**Mabadiliko ya msingi kwenye Kanuni katika toleo la 2.0 yanajumuisha mada zifuatazo tatu:**

- Uimarishaji wa jukumu la kijamii na miongozo ya haki za binadamu na haki za wafanyakazi.
- Mwongozo wa uhakiki wa data za ufuatiliaji na operesheni za uwazi.
- Kutumika katika viwanda, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs), na wadau wengine wanao fanya ufuatiliaji.

***Mwongozo wa Uimarishwaji wa Uwajibikaji wa kijamii na haki za wafanyakazi:***

Toleo la 2.0 linajumuisha marekebisho katika uwajibikaji kwa jamii na lugha ya haki za binadamu na wafanya kazi ambazo zinatoa taswira ya mapitio makubwa yaliyofanywa na wataalamu katika uwanja huo.

Kupitia mifumo ya eCDT pekee haiwezi kuboresha mazingira ya wafanyakazi baharini, mchango wao katika ufuatiliaji wa haki za binadamu unategemea watu kuwa na imani katika uhalali wa data, ambapo hili linasisitiza umuhimu wa mazoea ya kuhakiki data, na matumizi ya data kwa maamuzi ya kisheria na hatua za kuingilia kati. Kutokana na sababu hizi, FishWise iliweka mwongozo zaidi namna serikali zinavyopaswa kushughulikia ushiriki wa wafanyakazi na uhifadhi wa taarifa za wafanyakazi. Marekebisho zaidi kwenye hatua za Njia hizi yanaweza kutarajiwa, kubadilika kadri miongozo inavyoendelea kuwa ya kimaadili kwa matumizi ya data kusaidia haki za binadamu na haki za wafanyakazi.

***Mwongozo wa uthibitishaji wa data za ufuatiliaji na operesheni za uwazi:***
Kanuni za 2.0 zinajumuisha nyenzo za ziada na mwongozo wa kusaidia uthibitishaji wa data ya ufuatiliaji, uwajibikaji wa mtumiaji na operesheni za uwazi. Ingawa programu za eCDT ni muhimu sana katika kutoa mwonekano katika minyororo ya usambazaji wa mazao ya bahari kwa ufuatiliaji ulio boreshwa, operesheni, kuhakikisha usitawi wa binadamu, na manufaa mengine mengi, uthibitishajii wa data ili kuhakikisha utekelezaji wa maamuzi halali ni muhimu vile vile. Ufuatiliaji uliofanikiwa hauhitaji bidii tu katika namna data inavyokusanywa, lakini uhakikisho wa usahihi na madhumuni yake ya kushirikisha data, pamoja na uwajibikaji kwa matumizi sahihi na uhifadhi wa data kwa wakati unaofaa na kwa uwajibikaji. Uwazi kuhusu umuhimu wa matumizi ya programu, michakato ya kufanya maamuzi, na itifaki za kushirikisha data ni muhimu ili kuhakikisha kuwa watu wanaohitaji ufikiaji kupata taarifa za minyororo ya usambazaji wana zipata, wakati huo huo kuzingatia masuala ya faragha na umiliki wa data. Uwazi, uwajibikaji na uthibitishaji ni muhimu kwa ufuatiliaji.

***Kutumika katika viwanda, NGOs, na wadau wengine wa ufuatiliaji:***
Ingawa muundo na utekelezaji kamili wa programu ya eCDT unahitaji usaidizi wa serikali, kukubalika, na matengenezo ya muda mrefu, kuna hatua ambazo sekta za viwanda na mashirika yasiyo ya kiserikali yanaweza kuchukua ili kuanzisha kuunda programu (kama vile kutambua wadau, ushirikishaji wa chini kwenda juu, upeo wa kiteknolojia, n.k.) ili kuzalisha nia ya kisiasa na kuimarisha utayari wa kuwekeza. Kanuni 2.0 inajumuisha masasisho kadhaa ya kupanua utumiaji huu.


Photo Credit moodboard adobestock.com

# Utangulizi

Serikali ulimwenguni kote zinaendelea kutambua umuhimu wa kudumisha uwazi katika mnyororo wa usambazaji wa mazao ya bahari. Moja ya nyenzo turufu itumikanayo na serikali pamoja na makampuni binafsi ni kutegemea mifumo ya kidigitali yenye uwezo wa kufuatilia kwa uwazi mazao ya bahari katika mnyororo mzima wa thamani.

> **Ufuatiliaji na uhifadhi wa taarifa za mavuvi kwa njia ya kielektroniki ni kusambaza na kufuatilia taarifa za uchakataji/usindikaji na usafirishaji wa mazao ya bahari. Ukusanyaji wa data na usambazaji kwa njia ya kielektoriniki, unarahisisha unakilishaji na usambazaji wa taarifa kwa haraka na kuwezesha uthibitishaji wa serikali husika kwa ajiri ya matumizi mapana katika mnyororo wa usambazaji.**

Mitandao ya teknolojia inahusika kwenye ufuatiliaji wa kielektronikia na ina uwezo wa kuboresha ufanisi wa utendaji kazi katika mnyororo wa usambazaji kwa kuandaa taratibu za kuripoti na kufuata utaratibu wa makampuni yatakayo shiriki. Programu za ufuatiliaji zimeundwa ili kutumika katika udhibiti wa taarifa kwa kutumia mitandao ya teknolojia iliopo. Mipango ya ufuatiliaji inatekelezwa katika ngazi ya usimamizi wa uvuvi na serikali.

Endapo taarifa za kijamii, kiikolojia na kiuchumi zita ambatana na bidhaa za uvuvi serikali zinaweza kutumia taarifa hizo kuimarisha usimamizi na sharia za uvuvi katika kuunda usawa kwa wafanyakazi wa sekta ya uvuvi, pamoja na kuzuia bidhaa haramu, zisizo ripotiwa, na zisizodhibitiwa (IUU). Pamoja na hayo, bidhaa zisizo na lebo zitadhibitiwa kuingia katika minyororo ya usambazaji na masoko ya ndani na kimataifa. Data zilizo kusanywa kutoka kwenye programu ya eCDT zinaweza kuingia katika taasisi za kiserikali, mashirika yasio ya kiserikali na mifumo ya sekta ili kufanikisha malengo hayo.

> **Kutumia data iliyonaswa kutoka kwa programu za ufuatiliaji kusaidia malengo ya kiikolojia, kijamii, na kiuchumi kwa wakati mmoja huitwa mbinu za kina.**



Idadi ya nyaraka zilizopo kama vile miongozo ya hiari ya uhifadhi taarifa za mavuvi iliotolewa na shirika la chakula na kilimo duniani (FAO) au Mazungumzo ya Kimataifa kuhusu Ufuatiliaji wa Mazao ya Bahari (GDST)—Miongozo imebainisha njia madhubuti za mavuvi
katika kanda maalum, au aina ya vipengele muhimu vya data vya kukusanya. Ijapokua, hakuna jarida linalo jumuisha njia zote zilizo bora. Kuna uhitaji wakua na muongozo mpana unao jumuisha njia madhubuti za kufuatwa na serikali ili kuunda na kutekeleza programu ya ufuatliaji wa mazao ya bahari katika kufanikisha malengo endelevu ya (Kiikolojia, kijamii na kiuchumi). Pasipo muongozo huu, serikali inaweza kuunda mpango ambao unashughulikia tatizo moja tu!, kama vile mahitaji mapya katia soko la uingizaji bidhaa nchini. Matokeo yake, Serikali inaweza kukosa faida nyinginezo ambazo mpango wa eCDT unaweza kutoa.

Umoja wa Ufuatiliaji na Uhalalisho wa mazao ya bahari (SALT) uliratibu kamati ya mashauriano ambayo iliundwa na wadau 35 kutoka nchi 18 ili kushughulikia hitaji hili. Kamati iliainisha Kanuni sita za ufuatiliaji wa kielektroniki (eCDT) pamoja na miongozo ya kutumia. Kanuni hizo zinatumika kama njia bora za ufufatiliaji katika serikali za nchi zinazo zalisha mazao ya bahari wanapoelekea kwenye mbinu ya kina ya kuanzisha, kuunda, kutekeleza, na/au kuboresha programu zao za ufuatiliaji. Tangu kutekeleza Misingi na Njia na wadau wa serikali na sekta ya viwanda, tumepokea maoni kuhusu umuhimu wa mwongozo huu na tumeufanyia marekebisho ili kuzingatia uzoefu wa watumiaji, mabadiliko katika mazoea bora na rasilimali zinazoendelea, na mwongozo wa haki za binadamu na haki za wafanyakazi kwa matumizi ya programu za eCDT katika kutathmini hatari za kijamii.

Kimsingi Kanuni za eCDT ziliundwa kwa serikali za nchi zinazo zalisha mazao ya bahari au nchi zilizo chanzo cha mazao ya bahari. Lakini, SALT inatazamia kanuni hizo kuwa muhimu kwa juhudi za ufuatiliaji kwa wadau wengine (k.m., wavuvi, kampuni za mazao ya bahari, jamii, vikundi vya jamii/wafanya kazi na asasi zisizo za kiserikali, watoa huduma za teknolojia ya ufuatiliaji, na serikali za washirika. Wadau wasio wa serikali wanaweza kutumia mwongozo huu kuanzisha programu za eCDT na kujenga kukubalika kwa watumiaji ambao wanaweza kusaidia utayari wa kisiasa na hatimaye hatua za serikali.

**Kanuni ni za kiwango cha juu na wazi zenyekuwezesha ufumbuzi wa kiteknolojia na mikakati ya utekelezaji kufikia malengo ya nchi husika. Kanuni haziwasilishwi kwa utaratibu wowote wa kipaumbele, wala hazikusudiwi kuwa za mlolongo.**

Tembelea tovuti ya FishWise Kwa maelezo zaidi kuhusu kanuni, na nyenzo zinazofaa, tafiti, na mwongozo ambao umeshabihiana na kila hatua. Ikiwa una utayari wa kutumia Kanuni hizi kwa kazi yako, FishWise inaweza kukusaidia. Tufikie kupitia **SALT@FishWise.org**



# Kanuni za Ufuatiliaji

# Kanuni za Ufuatiliaji

## Muhtasari

Kuunda na kusimamia mpango wa kukusanya data muhimu zitokanazo na shughuli za uvuvi ni kazi ngumu kwa serikalii na makampuni. Lakini zikikusanywa, wadau wengi wanaweza kuchukua fursa ya taarifa hizi kushughulikia malengo ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi. Kujenga mbinu yenye matokeo matatu katika muundo na utekelezaji wa programu ya eCDT ya nchi husika, ni njia mojawapo ya kusaidia kufikia malengo haya yote.

Ili kurahisisha mchakato huu, Kanuni za Kina za eCDT ziliundwa. Huu ndio msingi wa kuzingatiwa katika mchakato mzima wa kuunda, kutekeleza, au kuboresha programu ya eCDT ili kufikia malengo ya kina (ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi). **Kanuni izi hazijawasilishwa kwa mlolongo wa kipaumbele; badala yake, taarifa zote zina umuhimu sawa na zinapaswa kuzingatiwa katika mchakato mzima.**

Kanuni hizi zinaweza kutumika kwa njia tofauti kulingana na jinsi serikali ipo tayari katika kutekeleza mpango wa programu hii ya ufuatiliaji wa kielektroniki eCDT (kama mfumo umeanzishwa au tayari kuna misingi thabiti inayo hitaji kuboreshwa). Kanuni hizi zina nyumbilika ili kuwezesha yeyote kuutumia kufikia malengo ya pamoja ya mfumo wa eCDT.

Ili kuwezesha watumiaji katika matumizi ya Kanuni hizi, Njia mtandaoni inayo elekeza juu ya Kanuni hutoa hatua zilizopendekezwa za namna ya utekelezaji wa Kanuni hizi katika vitendo. Njia hii inatoa maelekezo ya mchakato wa kuanzisha au kuboresha programu kamili ya ufuatiliaji katika awamu tatu: Kuanzisha, Kuunda, na Kutekeleza.



Photo Credit whitcomberd adobestock.com

SALT
SEAFOOD ALLIANCE FOR LEGALITY & TRACEABILITY

# Kanuni za Kina za Uhifadhi na Ufuatiliaji wa Mazao ya Bahari kwa njia ya Kielektroniki (eCDT)

### Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi

Kuelewa na kutambua ushirikiana wa kiikolojia, kijamii na kiuchumi katika programu ya eCDT ili kukuza faida za matumizi ya mbinu za kina. Kila programu ya eCDT itakuwa na viwango tofauti vya faida katika kila nyanja, lakini watumiaji wanapaswa kuepuka kupata faida kwa gharama ya maeneo mengine ya athari.

### Tumia data kuwasiliana na wafanya maamuzi

Wasilisha taarifa muhimu mikononi mwa watu sahihi kwa wakati unaofaa, ili waweze kuzifanyia kazi na kufanya maamuzi yanayo tokana na data wakati wa kubuni, kutekeleza na kuboresha program ya eCDT.

### Kuunda Programu iliyo ya kielektroniki, shirikishi na yenye usalama wa Data

Ongeza ufanisi katika sekta nzima ya mazao ya bahari kwa kuzingatia uboreshaji wa mifumo ya ufuatiliaji taarifa kutoka analogia kwenda digitali. Chagua teknolojia zinazo kidhi mahitaji ya data, usalama na ufaragha kwa wafanyakazi.

### Jumuika na shirikiana na wadau

Shirikiana tangu awali, mara kwa mara na wale watakao tumia programu ya eCDT wale watakao athiriwa nayo, na kuwaelimisha makundi yote ili kuimarisha.

### Tengeneza programu bora imara endelevu

Tengeneza na udumishe usaidizi wa programu ya eCDT— kisiasa, kifedha, na kwa watumiaji—ili iweze kukua zaidi ya awamu ya majaribio.

### Shughulikia mahitaji ya data na uthibitisho katika mnyororo wa thamani wa uvuvi

Mahitaji ya data na uthibitisho yanatofautiana kati ya wadau na katika vifundo vya mnyororo wa thamani. Tambua mahitaji haya ya kipekee huku ukizingatia jinsi ya kukusanya, kuhifadhi, na kushirikisha data huku wakizingatia sauti za wafanyakazi, kushirikisha wafanyakazi wakati wote wa mchakato, na kuunga mkono mipango inayo pewa kipaumbele na wafanyakazi.


https://fishwise.org/traceability-principles/

# Kuzifikia Kanuni

Njia ya kuzifikia kanuni hutoa mwongozo wa kutekeleza kanuni kwa vitendo. Inafafanua hatua maalum kutumia kanuni wakati wa kuunda, kutekeleza ama kuboresha mpango wa kina wa programu ya eCDT.

Awamu tatu za kufikia uanzishaji wa programu:

- **Kuanzisha**, inahusisha tafiti za awali, uwekaji wa lengo,na uhusishaji wa wadau;
- **Kuunda**, inahusisha kutambua teknolojia, kugawa majukumu, na kuunda mfumo rafiki wa kukuza programmu;
- **Kutekeleza**, inahusisha ufanyaji wa majaribio ya programu, kuizoea na kupanua wigo.




Mwongozo huu umegawanywa katika awamu hizi tatu ili kurahisisha usambazaji na kuruhusu mtu yeyote bila kujali yuko katika awamu gani kuona jinsi Kanuni hizi zinavyotumika. Kila kitendo kilichoangaziwa kwenye Njia ina walau Kanuni moja, ambayo inaoneshwa na ikoni.

Kupata taarifa zaidi na nyenzo muhimu, tembelea Njia ya Kanuni kwenye tovuti ya FishWise's website:
**https://fishwise.org/traceability-principles/apply-them/**

# Kuanzisha




| Kanuni | Hatua ya njia |
|---|---|
| Jumuika na shirikiana na wadau | **1. Fafanua malengo na ukubwa wa programu ya eCDT**<br>• Kwa kushauriana na wadau, fafanua malengo kwa uwazi (katika nyanja za kiikolojia, kijamii, na kiuchumi) ya programu kamili ya eCDT, na jinsi data itakavyotumiwa kuchochea mabadiliko (k.m.,, kupitia matumizi ya data, uhakiki, na uwazi wa namna data zinavo tumiwa). |
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **2. Tambua mapema changamoto zinazoweza kutokea kwa maisha marefu ya programu**<br>• Fikiria ni nani atakayelipa kuanzisha na kudumisha mfumo; ni motisha gani ya soko inaweza au haiwezi kuwa mahali; na uwezo wa kushawishi au kuimarisha utashi wa kisiasa.<br>• Tambua kama bajeti ya programu ni salama na ambapo msaada wa kisiasa ni nguvu na dhaifu zaidi. |

# Kuanzisha

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| Tumia data kuwasiliana na wafanya maamuzi | **3. Jifunze kutoka kwenye juhudi za eCDT zilizo fanyika**<br>• Kagua programu na mafunzo ya awali ya eCDT kuepuka kurudia makosa. Zingatia mapendekezo ya programu ya ufuatiliaji nje ya mazao ya bahari kuelewa mahitaji ya data.<br>• Kushauriana na mashirika yasiyo ya kiserikali ya eneo husika na/au washauri wa teknolojia ambao wanaweza kusaidia katika tathmini na juhudi za kujifunza kutoka kwa wenzao. |
| Tumia data kuwasiliana na wafanya maamuzi | **4. Fanya utafiti, tathmini, au uchambuzi wa gepu kwenye programu zilizopo na mazingira wezeshi ya kutambua mifumo inayounga mkono, utekelezaji na utayari wa kisiasa**<br>• Tambua na tathmini namna ya kufikia kile kilichopo ili kusaidia mpango wa kina wa eCDT (yaani; miundombinu, data na usanifu wa mifumo ya data, hatua za udhibiti, taasisi zinazovutiwa, au mipango husika ya sekta binafsi).<br>• Tathmini mitazamo ya wadau na kitaasisi juu ya uwezekano wa programu mpya kabisa, ikijumuisha athari zake za kijamii na kiuchumi (pamoja na gharama za kuendeleza, kupitisha, kutumia, n.k.) ili kupunguza athari zisizotarajiwa kama vile athari mbaya za mazingira au haki za binadamu.<br>    ◦ Changanua athari za programu ya eCDT kulingana na jinsia tofauti pamoja na makundi mengine muhimu ya wadau.<br>• Tumia ubia uliopo au kuhimiza uundaji wa ushirikiano kati ya serikali na wafanyabiashara ili makundi yote mawili yatekeleze vyema majukumu yao ya ziada kama ilivyoainishwa katika Kanuni Elekezi za Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Haki za Binadamu.<br>• Zingatia kanuni, sera, na utekelezaji wa serikali kuhusu afya na usalama, kanuni za msingi za haki za binadamu (k.m.,, mikataba ya msingi ya ILO, ushirikiano na vyama vya wafanyakazi vya kitaifa au kimataifa), na sauti za wafanyakazi ambazo huwezesha mifumo madhubuti ya malalamiko bila kulipiza kisasi, huku ikilindai usiri wa wafanyakazi, kukuza kazi zenye staha, na kuzingatia haki za msingi za binadamu na haki za wafanyakazi. |

# Kuanzisha

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| Tumia data kuwasiliana na wafanya maamuzi | **5. Tabia za mnyororo wa usambazaji**<br>• Andaa majumuisho yanayohusu uvuvi, ikiwemo kumbukumbu za mavuvi ya sasa, ripoti na mazoea ya kukusanya data ya uwajibikaji kwa jamii katika mashirika yote ya serikali.<br>• Kurahisisha upangaji wa data (wakati mifumo ya teknolojia inaweza kubadilishana taarifa au data kwa urahisi) kwa kutambua mahitaji ya data za wafanyakazi na bidhaa ambazo tayari zipo kwenye masoko muhimu na kati ya mamlaka husika (m.f., sheria za uingizaji, usalama wa chakula).<br>• Tambua miundo yoyote ya data sanifu ambayo inaweza kuwa muhimu kwa malengo ya programu (m.f., GDST KDEs). |
| Tumia data kuwasiliana na wafanya maamuzi | **6. Tathmini mapungufu na hatari zilizopo**<br>• Tathmini mapungufu na hatari ya uvuvi haramu, usioripotiwa, na usio na udhibiti (IUUF) kwa rasilimali na minyororo ya usambazaji inayofaa ndani ya programu ya eCDT, ikiwa ni pamoja na mbinu za kupunguza hatari zozote zilizotambuliwa, kama zipo.<br>  ◦ Taja bainisha maeneo ya hatari na mbinu zinazo hitajika kurekebisha masuala yaliyotambuliwa (m.f., udhibiti wa bandarini, uhakiki wa data, ukaguzi wa vyombo, kujengea uwezo wadau wa minyororo ya usambazaji, n.k.).<br>  ◦ Tambua mamlaka au idara zinazohusika na kuchukua hatua kuhusu mahitaji ya uboreshaji wa data au mchakato, na vizuizi vinavyoweza kuwa vya kuhusiana ikiwa mamlaka husika zitachagua kutoshiriki katika mpango wa eCDT.<br>• Tathmini hali ya uwazi na hatari zilizopo za unyanyasaji wa haki za kibinadamu kwa watu wanaofanya kazi au wanaohusishwa na mavuvi husika katika mnyororo wa thamani, ikiwa ni pamoja na kuwezesha mbinu za kuimarisha sera ya ulinzi wa wafanyakazi, kama vile haki ya kuhusishwa kwa uhuru na kujadiliana kwa pamoja, na ulinzi wa jumla wa kijamii, kama vile ulinzi wa uhuru wa kujieleza na utetezi wa haki za binadamu. |

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | ◦ Bainisha vyanzo na mahitaji ya data na hatari iliyopo, ikijumuisha muda unaotumika baharini, kumbukumbu za manahodha, au matukio ya usafirishaji ya baharini kwa baharini, mienendo ya uajiri na hatari kwa familia za wavuvi.<br>◦ Tambua asasi husika za kiraia, vyama vya wafanyakazi ikiwemo vyama vya biashara, mashirika ya usimamizi, au idara (kama vile Idara za Kazi au Ajira) zinazo shughuli za hatari za haki za binadamu, unyanyasaji, sera na/au ukusanyaji wa data. |
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **7. Kukusanya takwimu za kiuchumi kujiandaa kwa uchambuzi wa manufaa ya gharama**<br>• Kusanya gharama ya data za awali zinazohusika na mpango wa sasa wa usimamizi wa uvuvi, ikijumuisha usalama wa chakula na uzingatiaji wa kanuni.<br>• Weka matarajio ya muda mrefu yanayo shabiiana na faida inayo wezekana kwenye uwekezaji, kwa kuwa mapato ya kifedha yanaweza kuchukua muda kuonekana. |
| Jumuika na shirikiana na wadau | **8. Shiriki kuwatambua wadau**<br>• Tambua ipasavyo wadau kutoka serikalini, wavuvi walioathirika (ikiwa ni pamoja na wavuvi wadogo wadogo), watoa huduma za teknolojia, kampuni za usambazaji, vyama vya wafanyakazi, ushirikiano wa wadau mbalimbali, na vikundi vingine vya wafanyakazi/wakazi, iwe inalenga kubuni programu ya eCDT katika ngazi ya kimataifa, kitaifa, au kikanda inayokidhi mahitaji ya wadau hao.<br>• Bainisha kama programu itaathiri wadau walio na upungufu wa haki na wasiojiweza (ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wahamiaji na wanawake) na chukua hatua za kujenga uaminifu na kuwajumuisha. |
| Jumuika na shirikiana na wadau | **9. Elezea faida na motisha ili kuchochea ushiriki wa Wadau**<br>• Bainisha na eleza pendekezo la thamani la eCDT kwa ushirikiano na watumiaji wa programu (biashara, mashirika ya viwango na ubora, wanasayansi, wafanyakazi, n.k.). |

# Kuanzisha

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | • Kuwa mwazi kwa wadau kuhusu manufaa ya programu ambayo yameainishwa katika programu nyingine, upana wa program uliokusudiwa, na Kiwango cha ubadilishaji wa utekelezaji wa hiari wakati faida hazipatikani. |
| Jumuika na shirikiana na wadau | **10. Wasiliana na wadau mapema na mara kwa mara ukiwapa kipaumbele cha mahitaji yao**<br>• Tambua njia ya mawasiliano inayo pendelewa na makundi ya wadau waliohusika katika kuunda programu, na hakikisha usawa wa ushiriki katika makundi yaliyotengwa, na kunyimwa haki ambayo itategemea uwanda, malengo na sifa za mavuvi.<br>• Tumia maarifa na kujenga uwajibikaji na imani kwa kufuata njia na mbinu zinazopendelewa na wadau; tumia lugha ya eneo na muundo wa kueleweka, ukizingatia mahitaji ya watumiaji, tamaduni, na vikundi ambavyo vinaweza kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na utekelezaji wa eCDT.<br>• Zingatia nguvu na uhusiano miongoni mwa wadau katika mchakato wa mashauriano (k.m., wafanyakazi na wafanyabiashara, jinsia, serikali na sekta binafsi).<br>    ◦ Tumia mchakato shirikishi wa kufanya maamuzi ulio na uwazi.<br>    ◦ Jumuisha vyama vya wafanyakazi na wanachama wa jamii katika miundo ya utawala ili kuunga mkono mazungumzo ya kijamii ya muda mrefu.<br>• Hakikisha kwamba maoni kutoka kwa wadau yanajumuishwa katika kipindi chote cha maisha ya mradi ili kuboresha programu inavyo endelea. |

# Kuunda




| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| Shughulikia mahitaji ya data na uthibitisho katika mnyororo wa thamani wa uvuvi | **11. Ainisha mahitaji ya data na changamoto zake katika mnyororo mzima wa usambazaji**<br>• Fafanua msingi wa data unaohitajika ili kufikia malengo ya programu.<br>    ◦ Tambua wapi taarifa inahitajika na fafanua mahitaji ya data / teknolojia.<br>• Ainisha vipengele muhimu vya data (VMD) mpaka kwenye matukio muhimu ya ufuatiliaji (MMU) ndani ya minyororo ya thamani iliyotafsiriwa na.<br>    ◦ Utambue mahali ambapo(CTEs) yanayoanzia nakuishia kutokana mamlaka au tofauti kati ya wahusika tofauti (k.m., wadhibiti, washikadau, mashirika ya eneo).<br>• Tambua mahali ambapo taarifa iliyojirudia inaombwa na fanya kazi na wadau husika ili kupangilia maombi katika ufanisi. |

# Kuunda

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | • Punguza kuepuka ukusanyaji data kwenye programu ya eCDT, lakini eleza waziwazi mahali zilipo toka (k.m., wavuvi wadogo, ainka fulani za vyombo vya uvuvi, matukio ambayo ukusanyaji wa data unaweza kutumika didi wafanyakazi). |
| Shughulikia mahitaji ya data na uthibitisho katika mnyororo wa thamani wa uvuvi | **12. Tengeneza programu ya eCDT kwa kuzingatia uthibitisho ama hitaji na changamoto**<br>• Unda mwongozo wa kuhakiki ubora wa data na unaohusisha data na hatua ya uhakiki.<br>  ◦ Tambua eneo na namna data itahakikiwa ili kusaidia usahihi na utimilifu wa programu.<br>  ◦ Fikiria kuingia mikataba na wataalamu/washauri wa nje ili wafanye ukaguzi kwa jicho la nje/ la mtu wa tatu kwa lengo la kuongeza uaminifu kwa watumiaji wa mfumo lakini pia kuwasaidia katika hatua za ufanyaji maamuzi. |
| Shughulikia mahitaji ya data na uthibitisho katika mnyororo wa thamani wa uvuvi | **13. Hakikisha Usalama wa data namuongozo(itifaki) za kufikia**<br>• Eleza Kwa Usahihi, juu ya nani mwenye nafasi ya kuzifikia data, madhumuni ya kuzifkia, huku kuzingatia faragha ya mfanyakazi.<br>  ◦ Zingatia idhini iliyotolewa na mshiriki katika kufikia data. |
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **14. Tambua maeneo muhimu ya kufanya majaribio**<br>• Chagua mnyororo wa usambazaji ambao unaeleweka vizuri na maeneo yenye msaada wa(viwanda na mashirika yasiyo ya kiserikali).<br>• Kuwezesha (au kujenga) kupitia mfumo uliopo au uliowahi kuwepo wa ufuatiliaji wa mazao ya bahari, pale itakapo yawezekana, kuzuia kurudia rudia aina za miradi na kuhimiza matumizi sahihi ya rasilimali. |

# Kuunda

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **15. Unda programu ya eCDT yenye kufiti katika program mama za usimamizi wa mavuvi**<br>• Ili kufikia maamuzi yenye muafaka, tambua tofauti kati ya programu ya eCDT inayopendekezwa mkakati wa kitaifa wa kusimamia Mavuvi.<br>• Zingatia wasiojiweza kutoa mchango wowote katika muundo wa programu iliyopo, najinsi mitazamo na maoni yao inaweza kubadilisha muundo.<br>• Husisha ukusanyaji wa data na tathmini samaki baharini ili kuunganisha mipango iliyopo ya usimamizi wa uvuvi katika kuhakikisha usimamizi endelevu wa uvuvi na kukuza uhifadhi wa viumbe hai. |
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **16. Tambua namna ustawi wa wafanyakazi utakavyo fuatiliwa na kuungwa mkono**<br>• TambuaTaasisi za kiutawala zenye mamlaka juu ya data zinazohusiana na ustawi wa wafanyakazi na masuala ya usalama wa data (k.m., Idara za Ajira Na utekelezaji yakima cha chini cha mshahara, hali ya uhamiaji na mahitaji ya vituo vya afya) ili kuongeza uhalisia, uingizaji na ushirikiano wa data yoyote ya kijamii iliyokusanywa. Kupitia programu ya eCDT.<br>• Zingatia itifaki zilizopo katika kusambaza data za kijamii kwa mashirika ambayo husimamia taarifa za wafanyakazi, na kurekebisha au kuunda itifaki mpya kama kutakuwa na hitaji la kuboresha matokeo ya ustawi wa wafanyakazi. |
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **17. Utekelezaji wa ulinzi ili kupunguza Athari hasi za ukusanyaji wa takwimu kwa kuzingatia haki za wafanyakazi na Faragha zao**<br>• Angalia sheria zilizopo za faragha za data, na utambue michakato, mbinu au mipango mipya ya kujibu masuala ya faragha ili kuwatoa wasiwasi wa wadau/watumiaji kama vinavyo hitajika.<br>    ◦ Hakikisha taarifa iliogundulika kumwanika mtu inaondolewa mara moja katika maudhui yanayopelekwa kwa umma.<br>• Hakikisha wavuvi na wafanyakazi wengine wana uwezo wa kupata faragha za malalamiko yao na mifumo ya utatuzi. |

# Kuunda

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | ◦ Rejea kwenye utangulizi kupata ufafanuzi wa 'njia za malalamiko' na'Utatuzi/tiba.'<br>• Unganisha watekelezaji wa programu za eCDT na wadau kwenye ufuatiliaji wa haki, utetezi, na mashirika na mifumo ya usaidizi wa kijamii (k.m. vyama vya wafanyakazi, mashirika ya utetezi wa wahamiaji, watetezi wa haki za binadamu, na mashirika mengine ya kiraia) ili kuweka muktadha ya madhara yanayoweza kuwapata wafanyakazi.<br>◦ Zingatia asasi za kilia ambazo zinaweza kuwasaida wafanyakazi na watu watakaosaida katika ufanisi wa programu waweze kupata mahitaji muhimu ya haki za binadamu (uhuru wa kutoa maoni na huduma za kitabibu) kwa kwa kusaidia kulinda haki za wafanyakazi, ambayo mara nyingi inahitaji ujuzi na uzoefu maalum. |
| Kuunda Programu iliyo ya kielektroniki, shirikishi na yenye usalama wa Data | **18. Tafuta kupunguza gharama**<br>• Zingatia gharama ndogo katika kuanikiza matumizi ya tekinolojia na katika ukusanyaji wa data ili kufikia madhumuni ya programu.<br>• Tambua teknolojia zinazoongeza thamani kibiashara' msingi uzingatiwe katika; kuhakikisha kuna muundo yakinifu wa kurejesha gharama zilizotumika. |
| Kuunda Programu iliyo ya kielektroniki, shirikishi na yenye usalama wa Data | **19. Zingatia dhima ya biashara na hatua zilizo chukuliwa**<br>• Hakikisha kuwa programu inaendana na mahitaji ya ufuatiliaji wa waagizaji wakuu kama Marekani, Umoja wa Ulaya, na Japan.<br>• Shirikisha mataasisi yanayofuatilia biashara (m.f. WTO) ili kuepuka kuunda vizingiti/vikwazo katika biashara. |
| Jumuika na shirikiana na wadau | **20. Ainisha majukumu, wajibu na mahitaji ya washikiadau katika kuelekea utekelezaji wa programu**<br>• Tambua majukumu na mamlaka ya kila wakala kama kwakua inachangia katika malengo ya kina ya mpango wa eCDT. |

# Kuunda

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | • Tambua namna ya kuunganisha vyema michakato ya mashirika mbalimbali yanayohusika kwa ufanisi wa programu.<br>• Tambua ikiwa mashirika yanahitaji usaidizi wa kiufundi au kujengewa uwezo ili kuunda mfumo wa usimamizi wa data, na kama ni hivyo jinsi ya kupata usaidizi huo.<br>• Elezea wajibu na uwezo wa sekta binafsi na vyombo vya serikali, hususani mashirika ya kiserikali yanayotekeleza kanuni ikiwa ni pamoja na, ajira,usalama wa chakula (nani atakaye zibeba gharama? Nani atakusanya na kuhakikia data? Je hatua za uundaji zitahusisha mashirikiano baina ya serikali na viwanda?).<br>• Tambua vikundi vitakavyoweza kuchangia katika utambuzi wa majukumu, wajibu, na mahitaji ya wafanyakazi (m.f. Kamati za wafanyakazi, Vyama vya ushirika vya wavuvi, Vyama vya wafanyakazi, na asasi zingine za kiraia).<br>• Orodhesha wajibu wa watu binafsi, kampuni zinazokusanya, kuhakiki na kuwasilisha data.<br>• Tambua fursa kwa washikadau-hususani asasi za kiraia na taasisi za kidini-kwa ajira ya uangalizi wa programu na miundo ya kitawala. |
| Jumuika na shirikiana na wadau | **21. Tengeneza makubaliano kati ya taasisi kwa ajili ya kushirikishana taarifa na majukumu**<br>• Tambua wazi majukumu na mamlaka ya kila shirika kama yanahusiana na malengo ya mpango kamili wa eCDT.<br>• Zingatia makubaliano ya usambazaji wa takwimu, mikataba rasmi inayoelezea kwa undani data zinazokusanywa na kusambazwa pua ni kwa namna gani zinaweza kutumika, na nani na kwa manufaa gani.<br>• Tambua jinsi ya kuunganisha michakato bora ya mashirika mbalimbali yanayohusika kwa ufanisi wa programu.<br>• Kuamua ikiwa taasisi zinahitaji usaidizi wa kitaalamu au kujengewa uwezo ili kuunda mfumo wa usimamizi wa taarifa, na ikiwa ni hivyo, ni jinsi gani zinaweza kupata usaidizi huo. |

# Kuunda

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| Jumuika na shirikiana na wadau | **22. Hakikisha wadau kutoka kwa minyororo husika ya usambazaji wa nakubali rasmi kuunga mkono mpango wa eCDT**<br>• Zingatia vyote kati ya kujitolea na hatua za (utendaji, ufuatiliaji, udhibiti, na utekelezaji) katika minyororo yote ya usambazaji ili kufikia kudhibiti uvuvi wa IUU (Haramu, Usioripotiwa na Usiopimika) na ulinzi kwa manufaa ya wafanyakazi.<br>• Kuajiri washawishi kusaidia kupitishwa kwa programu (viongozi wa jamii, wakuu wa chama, mabingwa wa sekta, viongozi wa mawazo, viongozi muhimu wa serikali za mitaa) na kujaribu programu. |
| Kuunda Programu iliyo ya kielektroniki, shirikishi na yenye usalama wa Data | **23. Tambua teknolojia za eCDT ili kutimiza mahitaji ya ukusanyaji na uchambuzi wa data**<br>• Ruhusu ukusanyaji wa data, malengo ya programu, na hitaji la mtumiaji kuendesha uteuzi wa zana za eCDT itakayo hitajika, Sio kazi zilizoahidiwa za teknolojia yenyewe.<br>• Bainisha usanifu wa mfumo (k.m., hazina ya kati, leja iliyosambazwa).<br>• Hakikisha kuwa programu haifungamani na upande wowote, inapofaa, na kwamba mifumo ya uwazi (maombi ya umma ya mapendekezo, kwa mfano) ni ya ulazima wakati wa kushindania mikataba ya serikali. |
| Kuunda Programu iliyo ya kielektroniki, shirikishi na yenye usalama wa Data | **24. Unda programu na teknolojia za eCDT kupitia mbinu ya "muundo unao zingatia binadamu"**<br>• Tumia mbinu au miundo mahususi kulingana na sehemuhusika, inapowezekana programu hio inapaswa kusaidia mwingiliano na zingine.<br>• Shauriana na watumiaji wa teknolojia kabla na wakati wa utekelezaji (Rejea: sehemu ya 'Kuanzisha' sehemu).<br>• Tumia uundaji pamoja ili kutengeneza programu, hii inawapa umiliki watumiaji na watakubaliana nayo. |

# Kuunda

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| Kuunda Programu iliyo ya kielektroniki, shirikishi na yenye usalama wa Data | **25. Tanguliza/pendekeza/kipaumbele katika mwingiliano wa programu hii na programu zingine zilizopo za ufuatiliaji wa data**<br>• Imarisha uwekezaji uliopo na uliopangwa.<br>• Tumia fomati sanifu za data (yaani, KDEs).<br>◦ Zingatia upatanishi na viwango vya data vya sekta/viwanda (m.f, Viwango vya GDST na Vifaa) na mahitaji ya data ya kuagiza ya hali ya soko (k.m.,U.S. SIMP)  Kama kuna majukwaa ya kitaifa ya ufuatiliaji wa kielektroniki, yaruhusu kuingiliana na mifumo ya eCDT, ikijumuisha mifumo ya sekta ya binafsi.<br>• Kuza mwingiliano na programu zilizoenea katika nchi nyingine. |
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **26. Hamasisha upitishwaji wa Kanuni hizi katika sera**<br>• Himiza upitishaji/uendelezaji wa sera zinazokidhi viwango vya kimataifa vya data na sheria za uingizaji ili kuimarisha uungwaji mkono wa eCDT katika ngazi za kiserikali.<br>• Tetea kwa ajili ya kuidhinishwa kwa serikali na utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa zinazo sawazisha matarajio ya haki za wafanyakazi.<br>• Himiza mifumo na sera za ufuatiliaji wa wanunuzi kuunganishwa katika itifaki za programu kwa kushirikiana na washirika wa minyororo ya usambazaji, kuthibitisha madai ya ustahimilivu, kutekeleza mifumo inayoshirikiana, n.k.<br>• Kujenga msaada kutoka kwa jamii kwa programu pale inapowezekana kufanya hivyo. |
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **27. Kadiria kiwango cha fedha kinachohitajika na mgawanyiko wa fedha kulingana na shughuli ili kutengeneza programu endelevu**<br>• Tengeneza mpango wa bajeti wa muda mrefu ili kusaidia hatua zote za utekelezaji wa programu (m.f., Huduma za kimawasiliano na teknolojia, utekelezaji wa sheria, uratibu wa mashirika, ufikiaji, msaada wa miundombinu, ufuatiliaji n.k). |

# Kuunda

| Principle | Hatua ya njia |
| --- | --- |
| Tumia data kuwasiliana na wafanya maamuzi | **28. Panga kusimamia ipasavyo mpango wa eCDT**<br>• Tenga muda wa ufuatiliaji na urekebishaji, hasa kutoka kwa vyombo vinavyotoa uangalizi.<br>• Buni programu kwa mtazamo chanya wa kufikiria yaliombele kwa kurusu utumiaji wa teknolojia za kisasa zitakazo ibuka katika uchanganuzi wa data.<br>• Epuka kuagiza teknolojia maalum ili programu iweza kukabiliana na mabadiliko. |

# Kutekeleza




| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **29. Jaribisha programu ya eCDT kwa watumiaji mahususi, ikiwemo watendaji waliopo katika mnyororo wa usambazaji, taasisi za serikali, watafiti, pamoja na wataalamu (washauri)**<br>• Rasimisha ushirikiano baina ya watumiaji na wawezeshaji ambao watatangulia katika utekelezaji.<br>• Tambua na bainisha vizingiti na changamoto zinazoweza kutokea wakati wa kuanza kuzoea mfumo.<br>• Hatua ya utekelezaji kupokea na kujumuisha mirejesho kutoka kwa watekelezajii wa kwanza/awali.<br>• Hakisha usalama wa data unazingatiwa na kuimarisha. |
| Jumuika na shirikiana na wadau | **30. Kutoa msaada, maelekezo na ujuzi kwa watumiaji wa programu kwa kadri itakavyohitajika**<br>• Kutoa mafunzo kwa wadau walio katika mnyororo wa usambazaji.<br>    ◦ Himiza utumiaji wa programu sambamba na mafunzo na msaada katika kuimarisha au kufanya tathmini pamoja na udadavuzi wa data zilizokusanywa. |

# Kutekeleza

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | ◦ Husisha mafunzo yanayoshirikisha watendaji walioko katika jamii ili kuhakikisha taarifa zina jumuishwa na kulindwa.<br>• Tumia njia na tamaduni rafiki ili kuhakikisha taarifa zinapatikana katika muongozo rasmi.<br>• Kuwa miongoni mwao na kushirikiana na wadau. |
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **31. Fuatilia na kutathmini ufanisi wa programu ya eCDT kwa kuchambua data ili kuhakikisha madhumuni ya saikolojia, kijamii na kiuchumi yana fikika**<br>• Pima madhara ya kiuchumi na yasio ya kiuchumi katika kuiendea  programu ya eCDT kama vile maboresho/usanifushaji wa bei za bidhaa, ongezeko wa ushiriki wa wanawake kwenye mnyororo wa usambazaji katika shughuli za uvuvi, na uimarikaji wa jamii utokanao na ongezeko la kipato cha ziada kinachozalishwa kutokana na utumiaji wa programu ya eCDT. |
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **32. Kuandika gharama za utekelezaji wa programu ya eCDTna gharama za mradi katika undeshwaji wa muda mrefu**<br>• Fanya tathmini ya gharama za uendeshaji kwa kutumia data za tafiti za kiuchumi kama Msingi.<br>• Fikiria kufanya utafiti wa athari za kiuchumi kwa mipango ya serikali kutetea ufadhili endelevu kutoka kwa bajeti za serikali.<br>• Tambua biashara zingine pamoja na vichocheo vya ukuaji wa viwanda (Kuwezesha, vipaumbele vya biashara, ufanisi wa uendeshaji, hali ya uhutaji katika soko).<br>• Zingatia kuandika na kusambaza taarifa zenye kuonyesha faida za mazingira, jamii na ikoloji. |
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **33. Tathmini Faida, vikwazo na changamoto za programu kwa kuzingatia usawa na ustawi wa wafanyakazi**<br>• Hakikisha na wezesha ushiriki wa mfanyakazi katika kuunda na kutekeleza programu ya eCDT. |

# Kutekeleza

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | • Fuatilia na tatua wasiwasi wowote unaoibuliwa na mfanyakazi kuhusiana ufanisi wa programu na masuala ya faragha.<br>• Fuatilia, tathmini na badilika kama itakavyoitajika.<br>• Tathmini Mpangilio na mwingiliano wa kimajukumu kati ya watekelezaji waprogramu ya eCDTc na taasisi ya kiserikali ayoratibuajira.<br>• Kuendeleakuimarishamidahalobainayawaendeshaji washughuliza uvuvinataasisiza kiajirailikuhakiki kuwadata zinazokusanywazinatumikakutekeleza sheria za haki za binadamu pamoja na faida nyingine za kijamii. |
| Kuongeza manufaa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi | **34. Fanya tathmini katika kutambua muda gani takwimu zinapaswa kukusanywa na kuchambuliwa kwa ajiri ya kusaidia maamuzi ya kusimamia mavuvuvi**<br>• Hakikisha mashirika muhimu yanakua na mtiririko mzuriwadata ili kuweza kufanya tathmini usimamizi wa mavuvi kwa kuzingatia hali ya mazingira. |
| Tumia data kuwasiliana na wafanya maamuzi | **35. Tumia zana za ufuatiliaji na tathmini ili kuchambua utendaji wa programu ya eCDT na kutambua fursa za usimamizi**<br>• Zingatia teknolojia ya kiwango kulingana na maoni ya mtumiaji. |
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **36. Elezea muhtasali na dhumuni la kuongeza**<br>• Tambua mshikadau inahusika na uwezeshaji wa kifedha pamoja na kutengeneza mfumo; ikiwa motisha ya soko ni endelevu; na utayari wa kisiasa unadumishwa. |
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **37. Kuainisha tofauti kati ya eneo la Mfanona na maeneo mengine kwa ajili ya utekelezaji**<br>• Changanua namna ambavyo dhumuni la programu hii ilio ongezwa namna inavyoingiliana na kutofautiana na ile ya mfano. |

# Kutekeleza

| Principle | Hatua ya njia |
|---|---|
| | • Chambua rasilimali za kukuza: je fedha, wafanyakazi, miundombinu, utayari wa kisiasa na rasilimali bado zipo na zina kadhi uwanda/ukubwa wa programu? |
| Tengeneza programu bora imara endelevu | **38. Rudi katika hatua ya kuanzisha na kuunda pale itakapohitajika hususani wakati wa ufuatiliaji na ufanyaji wa tathmini ya programu ya eCDT**<br>• Kiri ya kwamba data za programu zinahitaji, majukwaa ya teknolojia, na watumiaji au wanufaika wanaweza kubadilika na kuendana na hali ya mazoea bora ya tasnia, maendeleo ya teknolojia, shinikizo la soko, na upatikanaji wa mwongozo wa data ya binadamu na ustawi.<br>• Badilisha programu kulingana na muda ili kukidhi mahitaji mapya ya udhibiti, kijamii, kiuchumi, na kiikolojia. |

# Tumia Kanuni

## Tumia katika kazi yako

Hatua inayofuata nikujaribu nakutumia kwa kina kanuni za programu ya eCDT na utekelezaji. Kama unavutiwa kutumia kanuni hizi katika kazi zako, Ijulishe FishWise (Uvuvi wa busara) kwakua inaweza kukuwezesha kukamilisha jitihada zako. Tafadhali wasiliana nasi kwa kutuma maombi yako ili uweze kupata fursa yakujuzwa zaidi na kujadili juu ya fursa pamoja na kutambua vipaumbele na uhitaji wako.

Kama unamrejesho wowote au swali, wasiliana nasi kupitia:
**SALT@fishwise.org**.

